**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA THELATHINI NA NANE

**29 MEI, 2019**

# OROHDA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### KIKAO CHA THELATHINI NA NANE – TAREHE 29 MEI, 2019

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**316. MHESHIMIWA PROF. JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE (MWANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali inafanya juhudi kubwa katika kuendeleza elimu hapa nchini kwa kutoa elimu bure na hata kujenga Shule nyingi zikiwemo za Kata:-

Je, lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Maabara za Sayansi katika Shule zote za Kata nchini.

**317. MHESHIMIWA KITETO ZAWADI KOSHUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imeziagiza Halmashauri zote nchini kutenga asilimia tano ya Vijana na asilimia tano ya Wanawake kutoka mapato ya ndani ili kuchangia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Halmashauri ambazo hazizingatii takwa hilo.

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

**318. MHESHIMIWA KHADIJA NASSIR ALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Uzito mkubwa wa mwili ni dalili ya mwanzo ya magonjwa yasiyoambukiza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na magonjwa haya;

(b) Je, mbali na mazoezi ni mbinu gani nyingine za kitaalamu za kupambana na vitambi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**319. MHESHIMIWA AMINA SALEH MOLLEL (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali imejipangaje kutekeleza mojawapo ya malengo katika Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 wa Taifa 2016/2017, 2020/2021 katika kupanua wigo wa Utalii nchini *(diversification).*

**WIZARA YA MAJI:**

**320. MHESHIMIWA ANTHONY CALIST KOMU (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Serikali imetekeleza mradi wa maji katika Kata ya Mbokomu lakini maji mengi yanavuja barabarani na kusababisha kukosekana kwa maji maeneo mengi ya mradi kama vile Vijiji vya Korini Kusini, Kiwalaa na Korini Kaskazini:-

Je, kwa nini Serikali isihakiki ukamilifu wa mradi huo na kufanya marekebisho ikiwa ni pamoja na kubainisha waliohusika na kasoro zitakazobainika na kuwachukulia hatua stahiki.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**321. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Katika Bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali iliondoa kodi kwenye taulo za kike *(pads)* jambo ambalo ni muhimu sana kwa maisha ya Wanawake na Wasichana, mpaka sasa ni mwaka mmoja tangu kodi hizo ziondolewa lakini bei ya taulo za Kike haijashuka licha ya kuondolewa kwa kodi hizo nchi nzima:-

Je, ni lini Serikali itasimamia kwa ukamilifu suala hilo ili bei za taulo za Kike zishuke na kusaidia afya za Wanawake hususan Wasichana.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**322. MHESHIMIWA DANIEL NICODEMUS NSANZUGWANKO (KASULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Suala la kupima na kupanga Miji ni jukumu la Serikali:-

(a) Je, kwa nini Serikali isije na mkakati endelevu wa kupanga Miji yote ambayo imetangazwa kwenye Gazeti la Serikali;

(b) Je, kwa nini Serikali inatoa hoja nyepesi kwamba kazi ya kupima na kupanga Miji ni kazi ya Halmashauri wakati inajua kwamba Halmashauri nyingi nchini hazina nguvu ya kifedha kufanya kazi hiyo;

(c) Mji wa Kasulu ni Mkongwe; Je, ni lini Serikali itasaidiana na Halmashuri ya Mji wa Kasulu kupanga Mji huo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**323. MHESHIMIWA HAJI KHATIB KAI (MICHEWENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni sifa gani anastahili kuwa nazo Askari Polisi ili aweze kuteuliwa kuwa OCD.

**324. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Eneo la Rubwera Kata ya

Kyerwa ndio Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengi yalikuwa ya Wananchi lakini kuna eneo lilichukuliwa na Jeshi la Magereza na Wananchi wakazuiliwa kufanya shughuli yoyote kwenye eneo hilo:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi hao kama walivyoahidiwa.

**325. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwaeleza watanzania hususan Vijana kuwa ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuwabaini, kuwachunguza na hatimaye kuwafikisha Mahakamani wale wote waliobainika kujihusisha na mtandao wa biashara za Dawa za Kulevya;

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wakuwasaidia Vijana waliotumbukia kwenye dimbwi la matumizi ya Dawa za Kulevya.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**29 MEI, 2019** **KATIBU WA BUNGE**